**SHERIA YA KUFUTA SHERIA YA MAHKAMA YA KADHI NAM. 3 YA 1985 NA KUANZISHA UPYA MAHKAMA YA KADHI NA KUWEKA MASHARTI MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO**

## MPANGILIO WA VIFUNGU

**VIFUNGU** **MAELEZO**


**SEHEMU YA KWANZA**
**VIFUNGU VYA AWALI**

1. Jina fupi na kuanza kutumika.
2. Ufafanuzi.

**SEHEMU YA PILI**
**KUANZISHWA, MUUNDO, MAMLAKA NA USIMAMIZI WA MAHKAMA YA KADHI**

3. Kuanzishwa kwa Mahkama za Kadhi.
4. Muhuri wa Mahkama.
5. Mamlaka ya Mahkama ya Kadhi.
6. Sheria ya Ushahidi.
7. Kanuni za Taratibu na Utendaji kazi.
8. Kadhi Mkuu na Naibu Kadhi Mkuu.
9. Muda wa Utumishi wa Kadhi Mkuu na Naibu Kadhi Mkuu.
10. Kadhi wa Rufaa.
11. Kadhi wa Wilaya.
12. Mrajis wa Mahkama ya Kadhi.
13. Uwezo na kazi za Mrajis.
14. Mahkama ya Kadhi wa Rufaa.

15. Rufaa kutoka Mahkama ya Kadhi wa Rufaa.

16. Mahkama ya Kadhi wa Wilaya.

17. Mamlaka ya Mahkama ya Kadhi wa Wilaya.

18. Rufaa.


## SEHEMU YA TATU
## USULUHISHI


19. Uwezo wa kutoa amri na maelekezo ya kumaliza kesi.

20. Uwasilishaji wa kesi kwa usuluhushi.

21. Kazi za Msuluhishi.

22. Haki ya Wadaawa katika Usuluhishi.

23. Usiri.

24. Muda wa Usuluhishi.

25. Kuondoa mgogoro katika usuluhishi.

26. Mwisho wa Usuluhishi.

27. Usuluhishi ukishindikana.


## SEHEMU YA NNE
## MASHARTI YA JUMLA


28. Bajeti na Fedha za Mahkama ya Kadhi.

29. Lugha ya Mahkama ya Kadhi.

30. Kudharau Mahkama ya Kadhi.

31. Ushiriki wa Wakili au Vakili.

32. Kukubaliwa kwa Wakili na Vakili.

33. Kinga kwa Makadhi na maofisa.

34. Kufutwa na kubakiza.

**SHERIA NAMBA 9 YA 2017**

**NIMESAINI**

Alhemi

**{DR. ALI MOHAMED SHEIN}**
**RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI**
**WA BARAZA LA MAPINDUZI**

**...1 Novemba..., 2017**

# SHERIA YA KUFUTA SHERIA YA MAHAKAMA YA KADHI NAM. 3 YA 1985 NA KUANZISHA UPYA MAHKAMA YA KADHI NA KUWEKA MASHARTI MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

---

**IMETUNGWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

## SEHEMU YA KWANZA
## VIFUNGU VYA AWALI

Jina fupi na kuanza kutumika.

**1.** Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Mahkama ya Kadhi ya 2017 na itaanza kutumika mara tu baada ya kutiwa saini na Rais.

Ufafanuzi.

**2.** Katika Sheria hii, isipokuwa kama itaelezwa vyenginevyo:

"Kadhi" maana yake ni Kadhi Mkuu, Naibu Kadhi Mkuu, Kaimu Kadhi Mkuu, Kadhi wa Rufaa na Kadhi wa Wilaya;

"Jaji Mkuu" maana yake ni Jaji Mkuu wa Zanzibar na inajumuisha Kaimu Jaji Mkuu;

"Kadhi Mkuu" maana yake ni mtu aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 8 cha Sheria hii kuwa kiongozi mkuu wa Mahkama ya Kadhi;

"Mahkama ya Kadhi" inajumuisha Mahkama ya Kadhi wa Rufaa na Mahkama ya Kadhi wa Wilaya, kama ilivyoelezwa katika kifungu cha 3 cha Sheria hii;

"Mrajis" maana yake ni Mrajis wa Mahkama ya Kadhi aliyeteuliwa chini ya masharti ya kifungu cha 12 cha Sheria hii;

"Rais" maana yake ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;

"Sheria ya Kiislamu" maana yake ni mfumo wa Sheria ya Kiislam ambao msingi wake ni Quran, Hadith, Ijmaa na Qiyas;

"Ulamaa" maana yake ni mtu aliyeteuliwa kuwa Ulamaa chini ya Sheria ya Ofisi ya Mufti Nam. 9 ya 2001;

"Vakili" maana yake ni mtu aliyeruhusiwa na mwenye leseni ya kufanya kazi ya Uvakili katika Mahkama ya Kadhi na Mahkama ya Mwanzo, chini ya masharti ya Sheria inayosimamia mfumo unaoruhusu watu kufanyakazi za uwakili;

"Tume ya Utumishi ya Mahkama" maana yake ni Tume ya Utumishi ya Mahkama iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 102 cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984;

"Wadaawa" maana yake ni mdai na mdaiwa katika shauri la Mahkama ya Kadhi;

"Wakili" maana yake ni mtu yeyote ambaye si Vakili, aliyeruhusiwa kufanya kazi ya uwakili Mahkama Kuu ya Zanzibar na Mahkama zilizo chini yake, kwa mujibu wa masharti ya Sheria inayosimamia mfumo unaoruhusu mtu kufanya kazi ya uwakili;

"Waziri" maana yake ni Waziri anayehusika na mambo ya sheria.

## SEHEMU YA PILI
## KUANZISHWA, MUUNDO, MAMLAKA NA USIMAMIZI WA MAHKAMA ZA KADHI

Kuanzishwa kwa Mahkama za Kadhi.

**3.**-(1) Kunaanzishwa Mahkama itakayojulikana kama Mahkama ya Kadhi.

(2) Mahkama ya Kadhi itaundwa na Mahkama ya Kadhi wa Wilaya na Mahkama ya Kadhi wa Rufaa.

(3) Mahkama ya Kadhi wa Wilaya itakuwa na mamlaka ya awali ya kusikiliza kesi za madai kama ilivyoelezwa kwenye kifungu cha 5 cha Sheria hii.

Muhuri wa Mahkama.

**4.** Mahkama za Kadhi zitakuwa na muhuri utaokuwa na sura ya kimahakama kama utavyoridhiwa na Jaji Mkuu.

Mamlaka ya Mahkama ya Kadhi.

**5.**-(1) Mahkama ya Kadhi itakuwa na mamlaka ya kipekee juu ya masuala yote ya kimadai na kesi zote ambazo Wadaawa ni Waislam kuhusiana na:

(a) Ndoa, talaka na mambo yote yanayohusiana na hayo;

(b) Nafasi ya wanandoa;

(c) Matunzo na malezi ya watoto;

(d) Wakfu au amana za kidini, hiba na msaada;

(e) Wasia na urithi;

(f) Mgawanyo wa mali ya wanandoa pale ambapo kuna uchangiaji halisi; na

(g) jambo jengine lolote ambalo Mahkama ya Kadhi imepewa mamlaka na Sheria nyengine yoyote kulishugulikia.

(2) Bila ya kuathiri masharti yaliyoelezwa katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, mtu yeyote ambaye si Muislam anaweza kufungua shauri katika Mahkama ya Kadhi dhidi ya Muislamu kwa mashauri ya madai yanayohusu Sheria ya Kiislam.

(3) Kila Kadhi atakuwa na mamlaka ya kusikiliza kosa lolote la kudharau Mahkama lilofanywa kuhusiana na ofisi yake na atakuwa na uwezo wa kutoa adhabu kwa mujibu wa Sheria hii.

Sheria ya Ushahidi.

**6.** Sheria na Kanuni za ushahidi zitakazotumika katika Mahkama za Kadhi zitakuwa ni zile tu zinazotumika katika Sheria ya Kiislam.

Kanuni za Taratibu na Utendaji kazi.

**7.** Jaji Mkuu kwa kushauriana na Kadhi Mkuu, atatunga Kanuni za utaratibu na utendaji wa kazi utakaotumika katika Mahkama ya Kadhi.

Kadhi Mkuu na Naibu Kadhi Mkuu.

**8.**-(1) Kutakuwa na Kadhi Mkuu na Naibu Kadhi Mkuu watakaoteuliwa na Rais kutokana na mapendekezo ya Baraza la Ulamaa.

(2) Kadhi Mkuu na Naibu Kadhi Mkuu, kabla ya kuanza kutekeleza majukumu yao watakula kiapo mbele ya Rais.

(3) Kadhi Mkuu atakuwa ndiye Mkuu wa Mahkama ya Kadhi na atakuwa na wajibu wa usimamizi wa mambo yote ya Mahkama ya Kadhi.

(4) Naibu Kadhi Mkuu atakuwa ndiye msaidizi mkuu wa Kadhi Mkuu na atafanya kazi nyengine kama atakavyopangiwa na Kadhi Mkuu.

(5) Mtu atafaa kushika au kukaimu Ofisi ya Kadhi Mkuu au Naibu Kadhi Mkuu ikiwa ni muumini na mfuasi wa dini ya Kiislam na:

(a) Muadilifu na mwenye kuheshimika;

(b) Mwenye kiwango cha elimu cha angalau Shahada ya Kwanza ya Sheria ya Kiislam kutoka chuo kikuu kinachotambulika;

(c) mwenye uzoefu wa angalau miaka saba kuhusiana na masuala ya Sheria ya Kiislam; na

(d) mwenye taaluma na uzoefu wa dini unaolingana na sifa za kuteuliwa kuwa Kadhi.

(6) Rais anaweza, baada ya kushauriana na Jaji Mkuu, kumteua Naibu Kadhi Mkuu kuwa Kaimu Kadhi Mkuu iwapo itatokea:

(a) nafasi ya Kadhi Mkuu itakuwa wazi;

(b) Kadhi Mkuu yuko likizo au yupo nje ya Tanzania; au

(c) Kadhi Mkuu atashindwa kutekeleza kazi yake kwa sababu yoyote.

(7) Mtu aliyeteuliwa kuwa Kaimu Kadhi Mkuu, atapewa nguvu na madaraka kamili ya Kadhi Mkuu na atafanya kazi za Kadhi Mkuu mpaka atakapoteuliwa Kadhi Mkuu mpya au mpaka Kadhi Mkuu aliyekuwa likizo au aliyekuwa hawezi kufanya kazi atakapoweza na kurejea kazini.

Muda wa Utumishi wa Kadhi Mkuu na Naibu Kadhi Mkuu.

**9.** -(1) Kadhi Mkuu na Naibu Kadhi Mkuu atabaki katika nafasi yake mpaka atakapofikia umri wa miaka sitini ambapo anaweza kustaafu kwa hiari au miaka sitini na tano ambapo atastaafu kwa lazima.

(2) Bila ya kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Rais anaweza kuongeza muda wa utumishi wa Kadhi Mkuu na Naibu Kadhi Mkuu kama atakavyoona inafaa lakini muda huo hautozidi miaka mitano.

Kadhi wa Rufaa.

**10.**-(1) Mahkama ya Kadhi wa Rufaa itakuwa na Kadhi Mkuu, Naibu Kadhi Mkuu na Makadhi wengine wa Rufaa wasiozidi watatu watakaoteuliwa na Rais baada ya kupendekezwa na Baraza la Ulamaa.

(2) Kadhi wa Rufaa hatoanza kazi za ofisi yake mpaka ale kiapo cha utii na kiapo chengine cha utekelezaji wa kazi zake kama ilivyoelezwa na sheria.

(3) Mtu atakuwa na sifa za kuteuliwa kuwa Kadhi wa Rufaa ikiwa ni muumini na anafuata dini ya Kiislam na ana sifa za kuwa Kadhi Mkuu au Naibu Kadhi Mkuu.

Kadhi wa Wilaya.

**11.**-(1) Kutakuwa na Kadhi wa Wilaya katika kila Wilaya ambaye atateuliwa na Jaji Mkuu baada ya kushauriana na Baraza la Ulamaa.

(2) Kadhi wa Wilaya hatoanza kazi zake mpaka ale kiapo cha utii na kiapo chengine cha utekelezaji kazi zake mbele ya Jaji Mkuu, kama ilivyoelezwa katika Sheria hii.

(3) Mtu atafaa kuteuliwa kuwa Kadhi wa Wilaya ikiwa ni mfuasi wa dini ya Kiislam na:

(a) muadilifu na mwenye kuheshimika;

(b) ana angalau Shahada ya Kwanza ya Sheria ya Kiislam kutoka chuo kikuu kinachotambulika; na

(c) awe na uzoefu wa angalau miaka mitano katika masuala ya Sheria ya Kiislam.

Mrajis wa Mahkama ya Kadhi.

**12.**-(1) Inaanzishwa Afisi ya Mrajis wa Mahkama ya Kadhi ambaye atateuliwa na Tume ya Utumishi ya Mahkama baada ya kupendekezwa na Kadhi Mkuu.

(2) Mrajis wa Mahkama ya Kadhi atawajibika kusimamia utawala wa Mahkama za Kadhi.

(3) Mtu atafaa kuteuliwa kuwa Mrajis wa Mahkama ya Kadhi ikiwa:

(a) ameteuliwa au ana sifa ya kuteuliwa kuwa Kadhi wa Wilaya; na

(b) ana uzoefu wa angalau miaka mitano katika shughuli za Mahkama.

Uwezo na kazi za Mrajis.

**13.**-(1) Mrajis wa Mahkama ya Kadhi atakuwa na uwezo wa kutekeleza kazi zifuatazo:

(a) kutekeleza baadhi ya uwezo na wajibu wa Kadhi, na kusoma hukumu ya Mahkama ya Kadhi kwa maelekezo ya Kadhi Mkuu;

(b) kutoa amri na kufanya shughuli za Mahkama ya Kadhi zikiwemo:

(i) kufungua rufaa, mapitio au marudio ya kesi;

(ii) kutoa na kutuma taarifa ya wito wa Mahkama;

(iii) kuahirisha kesi;

(iv) kushughulikia ombi linalohusu malipo ya hukumu kwa awamu;

(v) kuondoa na kurekebisha rufaa, mapitio na marudio; na

(vi) malipo ya gharama za kesi na kusimamia utekelezaji hukumu.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Kadhi Mkuu kwa kushauriana na Jaji Mkuu, atampangia kazi na kumpa uwezo wa kutekeleza kazi nyengine Mrajis wa Mahkama ya Kadhi.

(3) Mrajis wa Mahkama ya Kadhi ataendesha na kusimamia viapo kwa mujibu wa Sheria ya Kiislamu.

(4) Mrajis wa Mahkama ya Kadhi atakuwa na uwezo unaolingana na uwezo wa Mrajis wa Mahkama Kuu kuhusiana na rufaa, marudio na ombi litakaloletwa kwa ajili ya kusajiliwa.

(5) Mtu yeyote asiyeridhika na amri yoyote ya Mrajis wa Mahkama ya Kadhi (isipokuwa usomaji hukumu au amri iliyopitishwa na Kadhi) anaweza kuomba kupinga amri hiyo kwa Kadhi wa Rufaa kwa njia ya maombi, yakiambatanishwa na kiapo kadiri itakavyokuwa.

(6) Kadhi Mkuu, Naibu Kadhi Mkuu au Kadhi wa Rufaa, atakuwa na uwezo kufuatilia ombi la mtu yeyote aliyeathirika na ombi hilo, kutengua amri au uamuzi

uliopitishwa na Mrajis wa Mahkama ya Kadhi, na kutoa hukumu au amri nyengine ya haki.

(7) Ombi lililofanywa chini ya kifungu kidogo cha (6) cha kifungu hiki, litawasilishwa ndani ya siku thelathini tokea amri au uamuzi kutolewa, au muda mwengine kama Kadhi Mkuu atavyoruhusu.

(8) Ombi hilo halitozuia kuendelea kusikilizwa kesi ya msingi au utekelezaji wa hukumu yoyote isipokuwa kama Mrajis wa Mahkama ya Kadhi, Kadhi Mkuu, Naibu Kadhi Mkuu au Kadhi wa Rufaa ataamuru vyenginevyo.

Mahkama ya Kadhi wa Rufaa.

**14.**-(1) Kutakuwa na Mahkama ya Kadhi wa Rufaa ambayo itakuwa na mamlaka ya rufaa na mapitio kwa hukumu na maamuzi yanayotoka Mahkama ya Kadhi wa Wilaya.

(2) Katika kutekeleza mamlaka yake ya rufaa na mapitio, Mahkama ya Kadhi wa Rufaa itaongozwa na Kadhi Mkuu, Naibu Kadhi Mkuu au Kadhi wa Rufaa kama itakavyoamuliwa na Kadhi Mkuu.

(3) Katika kutekeleza mamlaka yake, Mahkama ya Kadhi wa Rufaa itakuwa na uwezo wa:

(a) Kukubaliana au kutengua hukumu, maamuzi na amri za Mahkama ya Kadhi wa Wilaya;

(b) kuamuru kusikilizwa upya kwa kesi yoyote iliyosikilizwa na kutolewa uamuzi katika Mahkama ya Kadhi wa Wilaya; au

(c) kurejesha kesi yoyote iliyosikilizwa na kuamuliwa katika Mahkama ya Kadhi wa Wilaya ikiwa na maelekezo ya mwenendo wa ziada kama Kadhi Mkuu atakavyoona inafaa.

Rufaa kutoka Mahkama ya Kadhi wa Rufaa.

**15.**-(1) Rufaa au marudio kutokana na hukumu yoyote ya Mahkama ya Kadhi wa Rufaa itafunguliwa Mahkama Kuu.

(2) Katika kutekeleza uwezo wake wa rufaa na marudio, Mahkama Kuu itaundwa na Jaji wa Mahkama Kuu na Jopo la Ulamaa wanne wa Kiislam.

(3) Ulamaa watateuliwa na Mrajis wa Mahakama ya Kadhi miongoni mwa watu watakaopendekezwa na Baraza la Ulamaa.

(4) Kwa kuzingatia masharti ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, maamuzi ya Mahkama Kuu yatakuwa ya mwisho.

(5) Jaji anayekaa Mahkama Kuu chini ya kifungu hiki anatakiwa awe Muislam mwanamme.

(6) Katika kuteua Maulamaa wa Kiislam chini ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, Mrajis atazingatia madhehebu ya Wadaawa.

(7) Uamuzi wa Mahkama Kuu kuhusiana na kesi za Mahkama ya Kadhi utapaswa kufuatwa na kuzingatiwa na Mahkama zote za Kadhi, isipokuwa kwamba, katika kuitumia hukumu hiyo kama marejeo, madhehebu ya Wadaawa yatazingatiwa.

(8) Wakati wa kushughulikia rufaa, Jopo la Mahkama Kuu linaweza kumualika mtu yeyote mwenye taaluma na mtambuzi wa jambo linalohusika kama rafiki wa Mahkama.

Mahkama ya Kadhi wa Wilaya.

**16.**-(1) Jaji Mkuu anaweza kuanzisha katika kila Wilaya ya Zanzibar, Mahkama ya Kadhi wa Wilaya ambayo itakuwa na mamlaka ndani ya Wilaya ilipoanzishwa tu.

(2) Mahkama ya Kadhi wa Wilaya inaweza kufanya kazi zake sehemu yoyote kwenye eneo la mamlaka yake.

(3) Mahkama ya Kadhi wa Wilaya itaongozwa na Kadhi wa Wilaya.

Mamlaka ya Mahkama ya Kadhi wa Wilaya.

**17.** Mahkama ya Kadhi wa Wilaya itakuwa na itatekeleza mamlaka ya asili ya kusikiliza na kuamua mambo yote na kesi, kama zilivyoorodheshwa katika kifungu cha 5 cha Sheria hii.

Rufaa.

**18.** Rufaa kutokana na maamuzi ya Mahkama ya Kadhi wa Wilaya itapelekwa katika Mahkama ya Kadhi wa Rufaa.

## SEHEMU YA TATU
## USULUHISHI

Uwezo wa kutoa amri na maelekezo ya kumaliza kesi.

**19.**-(1) Bila ya kujali chochote katika Sheria hii, Mahkama ya Kadhi ya Wilaya inaweza ndani ya siku tano za kazi kuanzia tarehe ya kufunguliwa kesi, kwa uamuzi wake yenyewe, kumtaka Mdaawa yeyote au Wadaawa katika kesi kuhudhuria Mahkamani, ili Mahkama iweze kutoa amri kuhusu maombi ya muda yaliyofunguliwa au yanayokusudiwa kufunguliwa kwa ajili ya uendeshaji wa kesi kwa misingi ya haki, haraka na kwa gharama nafuu.

(2) Mahkama pia inaweza kuzingatia jambo lolote ikiwa ni pamoja na uwezekano wa kutatua mambo au jambo lolote katika kesi au mwenendo wa kesi, na

kuwataka Wadaawa kuwasilisha Mahkamani taarifa yoyote inayoonekana inafaa, na pia inaweza kutoa maelekezo yoyote yanayoonekana kuwa ni muhimu au yanafaa kwa ajili ya upatikanaji haki, utatuzi wa haraka wa kesi na unafuu wa gharama.

Uwasilishaji wa kesi kwa usuluhishi.

**20.**-(1) Iwapo kesi haijapata ufumbuzi chini ya sharti la kifungu kidogo cha (2) cha kifungu cha 21 cha Sheria hii, Mahkama ya Kadhi inaweza kuelekeza Wadaawa kuwasilisha kesi yao kwa ajili ya usuluhishi na baada ya kutoa maelekezo hayo, Mahkama itateua msuluhishi ambaye atapanga tarehe ya kuanza hatua za usuluhishi, isipokuwa kama Wadaawa kwa pamoja wamewasilisha tamko la kwamba usuluhishi hauhitajiki.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, msuluhishi atateuliwa miongoni mwa watu wenye kuheshimika, waadilifu na waelewa wa masuala ya dini ya Kiislamu na ambaye atakubaliwa na pande zote zinazohusika na shauri liliopo Mahkamani.

Kazi za Msuluhishi.

**21.**-(1) Katika kufanya usuluhishi chini ya Sheria hii:

(a) Msuluhishi atawawezesha Wadaawa kupunguza gharama na ucheleweshaji wa kazi ya usuluhishi, na atafanya usuluhishi wa haraka na kwa misingi ya haki;

(b) Msuluhishi atawezesha kuwepo mawasiliano baina ya wadaawa ili kuwasaidia katika kufikia suluhu inayokubaliwa na pande zote.

(2) Kwa mujibu wa masharti ya ujumla ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Msuluhishi:

(a) atapaswa, kwa uhuru na bila upendeleo kufanya kila linalostahiki kuwasaidia wadaawa katika kutatua mgogoro wao;

(b) anaweza, ikilazimika, kufanya mikutano ya pamoja au ya mtu mmoja mmoja, na anaweza kutoa mapendekezo ya kufikia suluhu;

(c) pale ambapo huduma ya mtaalamu inaweza kupatikana bila ya malipo au bila gharama, au pale ambapo huduma hiyo inaweza kupatikana kwa malipo, na ikiwa Wadaawa wakakubali kulipa gharama hizo, anaweza kupata ushauri wa mtaalamu katika vipengele vinavyohitaji utaalamu katika mgogoro huo na utaalamu huo utatolewa kwa uhuru na bila ya upendeleo.

(d) ataongozwa na misingi ya haki, usawa na misingi ya asili ya utoaji haki, na atazingatia pamoja na mambo mengine, haki na wajibu wa wadaawa, na mazingira yaliyouzunguka mgogoro wenyewe;

(e) anaweza, katika hatua yoyote ya utatuzi wa mgogoro huo na katika hali ambayo ataona inafaa, kuzingatia matakwa ya wadaawa, likiwemo ombi lolote kutoka upande wowote wa mzozo, kwa ajili ya utatuzi wa haraka wa mgogoro na kumtaka msuluhishi asikilize maelezo ya mdomo; na

(f) anaweza, katika hatua yoyote ya usuluhishi, kutoa mapendekezo kwa ajili ya utatuzi wa mgogoro.

(3) Pale ambapo Wadaawa wataafikiana wakati wa usuluhishi, Msuluhishi atayaweka maafikiano hayo katika maandishi na wadaawa watasaini hati ya maafikiano na Msuluhishi atasaini kama shahidi.

(4) Msuluhishi atawasilisha maafikiano hayo kwa Kadhi aliyepangiwa kesi inayohusika na usuluhishi huo.

Haki ya Wadaawa katika Usuluhishi.

**22.**-(1) Wadaawa katika kikao cha usuluhishi watakuwa na haki ya kutatua jambo lolote lililowasilishwa kwa ajili ya usuluhishi.

(2) Upande unaohitaji ridhaa ya upande mwengine kabla au baada ya kuanza kwa usuluhishi, utafanya mawasiliano na upande mwengine katika usuluhushi huo.

Usiri.

**23.** Mawasiliano yote katika vikao vya usuluhishi, nyaraka na kumbukumbu za usuluhishi yatachukuliwa kuwa ni siri, na baada ya hapo taarifa zozote zilizotolewa wakati wa usuluhishi hazitazingatiwa na hazitatumika kama ushahidi katika mwenendo wa kesi Mahakamani au juhudi nyengine za usuluhishi, isipokuwa kuhusiana na madai yaliyoletwa na mdaawa yeyote kutengua makubaliano ya suluhu kwa sababu ya udanganyifu.

Muda wa Usuluhishi.

**24.** Muda wa usuluhishi hautazidi siku kumi na nne kuanzia tarehe ya kikao cha kwanza cha upatanishi na ukihitajika muda wa ziada, muda huo ni lazima ukubaliwe na pande zinazohusika na usuluhishi.

Kuondoa mgogoro katika usuluhishi.

**25.**-(1) Ikiwa haiwezekani kuendesha usuluhishi kutokana na upande mmoja kutohudhuria vikao vya usuluhishi bila ya sababu za msingi au kutokana na sababu nyengine yoyote iliyo nje ya uwezo wa Msuluhishi, Msuluhishi anaweza kuondoa mgogoro katika usuluhishi na kuurejesha Mahakamani.

(2) Upande wowote usioridhika na amri iliyotolewa na msuluhishi chini ya kifungu hiki unaweza, ndani ya siku saba kuanzia tarehe ya amri hiyo, kuwasilisha Mahakamani ombi la kutaka kurejeshwa tena kwa Msuluhishi shauri lililoondolewa hapo awali.

(3) Baada ya kuridhika kwamba ada na gharama za usuluhishi zimelipwa kikamilifu, Msuluhishi atatengua uamuzi wake wa awali wa kuachana na usuluhishi, na kwa ridhaa ya Wadaawa wote wanaohusika, atatoa taarifa ya kuendelea na usuluhishi.

Mwisho wa Usuluhishi.

**26.** Usuluhishi utamalizika endapo:

(a) Msuluhishi atasitisha vikao vya usuluhishi kwa kukosa ushirikiano kutoka kwa Mdaawa, au pale ambapo Wadaawa wameshindwa kutii maelekezo ya usuluhishi;

(b) Wadaawa watasaini makubaliano ya usuluhishi;

(c) Msuluhishi atatoa tamko baada ya kushauriana na Wadaawa kwamba kuendelea na usuluhishi haiwezekani au hakuna maslahi;

(d) Wadaawa kwa pamoja watakubaliana kwamba usuluhishi usitishwe; au

(e) Mdaawa mmoja ametoa tamko kwa Msuluhishi na Mdaawa mwengine akakubali kwamba usuluhishi usitishwe.

Usuluhishi ukishin dikana.

**27.** Iwapo mpaka kufikia mwisho wa usuluhishi hakuna muafaka uliofikiwa, kesi itarejeshwa kwa Kadhi aliyepangiwa kuisikiliza, ambaye ataendelea kusikiliza kesi kuanzia pale kesi ilipopelekwa kwa msuluhishi.

## SEHEMU YA NNE
## MASHARTI YA JUMLA

Bajeti na Fedha za Mahkama ya Kadhi.

**28.** (1) Mahkama ya Kadhi itakuwa na Fungu lake la Bajeti ambamo mtaingizwa fedha zote zilizoidhinishwa au zitakazostahili kwa matumizi ya Mahkama ya Kadhi.

(2) Mlipaji Mkuu wa Serikali atateua afisa mhasibu kwa ajili ya Fungu la Bajeti ya Mahkama ya Kadhi na Mhasibu Mkuu wa Serikali atateua wafanyakazi wa kutosha kufanya kazi za kiuhasibu kwa ajili ya Fungu hilo.

(3) Fedha za Mahkama ya Kadhi zitajumuisha:

(a) fedha zilizoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi kila mwaka wa fedha kwa ajili ya matumizi ya Mahkama ya Kadhi;

(b) misaada, michango na fedha nyengine zilizopokelewa na Mahkama ya Kadhi kutoka vyanzo vyengine vinavyokubalika;

Lugha ya Mahkama ya Kadhi.

**29.**-(1) Mwenendo na kumbukumbu za mwenendo wa kesi zitakuwa kwa lugha ya Kiswahili.

(2) Endapo itatokea mdaawa si muelewa wa Kiswahili au ana ulemavu wa kuzungumza au ulemavu mwengine unaomzuia kuifahamu lugha ya Mahkama, Mahkama itatumia mkalimani.

(3) Kabla ya kuanza kazi yake ya ukalimani, Mkalimani ataapa mbele ya Mahkama ya Kadhi au Mrajis wa Mahkama ya Kadhi.

Kudharau Mahkama ya Kadhi.

**30.**-(1) Mahkama ya Kadhi itakuwa na mamlaka ya kuanzisha mashtaka dhidi ya mtu yeyote kwa kudharau Mahkama ya Kadhi na kwenye mashtaka hayo inaweza kuamuru faini isiyopungua shilingi laki tatu, au adhabu ya kifungo kisichopungua mwezi mmoja kwa mtu atakayepatikana na hatia ya kosa hilo.

(2) Mtu yeyote ambaye:

(a) akiwa katika eneo ambalo kazi za Mahkama zinaendelea, au ndani ya eneo linalotumika kwa kazi hizo, ataonesha dharau kwa maneno au vitendo kuhusiana na kesi inayosikilizwa, au kwa mtu yeyote ambaye yupo kwenye eneo ambalo kesi inaposikilizwa;

(b) akiwa ameitwa kutoa ushahidi katika kesi iliyopo Mahkamani na akashindwa kuhudhuria au anahudhuria lakini anakataa kuapishwa au kutoa uthibitisho, au bila sababu inayokubalika kisheria anakataa kujibu swali au kutoa hati, au anabakia katika chumba cha Mahkama baada ya kuamriwa kuondoka katika eneo hilo;

(c) anazuia au anasababisha usumbufu katika usikilizaji kesi;

(d) wakati shauri linaendelea, anatoa maneno au maandishi, yanayoweza kupotosha mwenendo wa kesi, au kumzuia mtu yeyote kwa maslahi au dhidi ya maslahi ya upande wowote wa kesi hiyo, au anadhalilisha mamlaka ya mtu yeyote ambaye kesi hiyo iko mbele yake;

(e) kinyume cha sheria, anajaribu kuingilia au kushawishi shahidi katika kesi;

(f) anafanya kitendo chengine chochote chenye nia ya kuonyesha dharau au kuharibu mwenendo wa kesi, au kwa mtu yeyote ambaye kesi hiyo anaisikiliza;

atakuwa ametenda kosa la kudharau mahakama na akipatikana na hatia atastahili kupewa faini isiyopungua shilingi laki tatu au adhabu ya kifungo kisichozidi mwezi mmoja au adhabu zote mbili kwa pamoja.

(3) Endapo kitendo cha kudharau Mahkama kimefanywa mbele ya Mahkama, haitakuwa lazima kwa Mahkama kutoa taarifa ya kumtaka kutoa maelezo ya kuonesha kwa nini hatua au shitaka lisifunguliwe dhidi yake, lakini Mahkama itahakikisha kwamba mtu anayetuhumiwa kudharau Mahkama analifahamu kosa lake, anapewa fursa ya kusikilizwa kwa kutoa utetezi wake, na kumbukumbu za mwenendo wa kesi zitatunzwa ipasavyo.

(4) Pale ambapo dharau ya Mahakama imefanywa nje ya Mahkama, taarifa ya kumtaka mshtakiwa kutoa maelezo ya kuonesha kwanini hatua au shtaka lisifunguliwe dhidi yake itatumwa kwa mtu anayetuhumiwa kufanya kosa hilo.

Ushiriki wa Wakili au Vakili.

**31.**-(1) Kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 32 cha Sheria hii, Wakili na wakala aliyeidhinishwa kisheria anaweza kuhudhuria kwa niaba ya upande wowote katika Mahkama ya Kadhi wa Wilaya, Mahkama ya Kadhi wa Rufaa, au Mahkama Kuu.

(2) Vakili na wakala aliyeidhinishwa kisheria wanaweza kuhudhuria Mahkama za Kadhi wa Wilaya na Mahkama ya Kadhi wa Rufaa pekee kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 32 cha Sheria hii.

Kukubaliwa kwa Wakili na Vakili.

**32.**-(1) Jaji Mkuu anaweza, kwa kushauriana na Kadhi Mkuu, kumruhusu Wakili au Vakili kusimamia kesi katika Mahkama ya Kadhi.

(2) Wakili au Vakili atakayeruhusiwa kusimamia kesi katika Mahkama ya Kadhi atatakiwa awe na elimu na uzoefu wa Sheria ya Kiislam.

(3) Jaji Mkuu ataweka utaratibu kwa Wakili au Vakili namna ya kuomba kuruhusiwa kusimamia kesi katika Mahkama ya Kadhi.

Kinga kwa Makadhi na maofisa.

**33.** Kadhi au mtu mwengine yeyote anayefanya kazi za Mahkama ya Kadhi, hatoshitakiwa katika Mahkama yoyote kwa madai au jinai kwa jambo lolote alilolifanya au kuamuru kufanywa katika utekelezaji wa majukumu yake, endapo wakati wa kufanya wajibu huo, alikuwa anafanya kwa nia njema huku akiamini kuwa ana mamlaka ya kufanya au kuamuru kufanywa jambo hilo.

Kufutwa na kubakiza.

**34.**-(1) Sheria ya Mahkama ya Kadhi Nam. 3 ya 1985 inafutwa.

(2) Bila ya kujali kufutwa kwa Sheria ya Mahkama ya Kadhi Nam. 3 ya 1985, mambo yote na kesi zote zinazoendelea katika Mahkama yoyote ya Kadhi chini ya masharti ya Sheria iliyofutwa, zitaendelea kusikilizwa na kutolewa uamuzi.

(3) Uamuzi au amri yoyote ya Mahkama yoyote ya Kadhi ambayo itakuwa haijatekelezwa au kutiliwa nguvu kabla ya Sheria hii kuanza kutumika, inaweza kutekelezwa na kutiliwa nguvu kama vile ni uamuzi au amri ya Mahkama iliyotolewa chini ya Sheria hii.

(4) Bila ya kujali kufutwa kwa Sheria ya Mahkama ya Kadhi Nam. 3 ya 1985, mambo na maamuzi yote yaliyofanywa chini ya Sheria iliyofutwa, yatachukuliwa kuwa yamefanywa chini ya Sheria hii.

(5) Bila kujali sharti lolote chini ya Sheria hii, Makadhi waliopo wataendelea kushikilia ofisi zao.

**UMEPITISHWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, tarehe 27 Septemba, 2017.

..................................................

(RAYA ISSA MSELLEM)

***Katibu wa Baraza la Wawakilishi***

***Zanzibar.***